Nation Media Group
Media of Africa for Africa

www.nationmedia.com
Nation Media Group | Nationmediagroup | @NationMediaGrp

# NATION MEDIA GROUP PLC

## ILANI KUHUSU MKUTANO MKUU WA MWAKA

Kutokana na janga lililopo la COVID-19 pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya Kenya chini ya Masharti ya Afya ya Umma (Uzuiaji, Udhibiti na Ufifishaji wa Covid-19), 2020 ambayo yanazuia mikutano na mikusanyiko ya watu, zikiwemo mbinu za kawaida za kufanya Mikutano Mikuu ya Wenyehisa mahali pamoja na kadhalika kulingana na kanuni za Sheria ya Kampuni, Namba 17 ya 2015 jinsi ilivyorekebishwa na Sheria ya Sheria za Biashara (Zilizorekebishwa) (Namba 2), 2021, Ilani inatolewa hapa kwamba Mkutano Mkuu wa Hamsini na Nane wa Mwaka wa wenyehisa wa shirika la Nation Media Group PLC utafanyika kwa njia ya mtandao saa tisa kamili siku ya Ijumaa, tarehe 25 Juni 2021 ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapa chini:

Maamuzi yote yataendeshwa kwa njia ya Kura ya Maoni.

**Kama shughuli ya kawaida inayofaa kuzingatiwa na, ikibainika kufaa, kupitisha maamuzi yafuatayo ya kawaida:**

**1.** Kupokea taarifa za kifedha za mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2020, na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi Wakuu na Wakaguzi zilizoambatishwa.

**2.** Kuthibitisha kuwa PricewaterhouseCoopers LLP wataendelea kuwa afisini kama Wakaguzi wa Mahesabu ya Kampuni hii kulingana na sehemu ya 721(2) ya Sheria ya Kampuni za Kenya 2015 na kuidhinisha wakurugenzi wakuu kubainisha malipo ya Wakaguzi wa Mahesabu.

**3.** Kuchagua na kuchagua tena wakurugenzi wakuu wafuatao:
- a) na Kifungu cha 110 cha Muafaka wa Maelewano wa Kampuni, Bw Dennis Aluanga anastaafu kwa mzunguko na kwa sababu anafuzu, anajitokeza ili kuchaguliwa tena;
- b) kulingana na Kifungu cha Muafaka wa Maelewano wa Kampuni, Bw Stephen Dunbar-Johnson anastaafu kwa mzunguko na kwa sababu anafuzu, anajitokeza ili kuchaguliwa tena;
- c) kulingana na Kifungu cha Muafaka wa Maelewano wa Kampuni, Bw Louis Otieno anastaafu kwa mzunguko na kwa sababu anafuzu, anajitokeza ili kuchaguliwa tena;
- d) kulingana na kanuni za sehemu ya 769(1) za Sheria ya Kampuni ya 2015, wakurugenzi wakuu wafuatao, wakiwa wanachama wa Kamati ya Ukaguzi wa Mahesabu ya pesa, Hatari na Udumishaji, wachaguliwe ili kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati hiyo;
  - i. Bw. Leonard Mususa
  - ii. Bw. Anwar Poonawala
  - iii. Bw. Al-Noor Ramji

**4.** Kupokea, kuzingatia na iwapo itabainika kuwa sawa, kuidhinisha Ripoti ya Malipo ya Wakurugenzi Wakuu pamoja na malipo yaliyotolewa kwa Wakurugenzi Wakuu katika mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2020, mbali na kuwapa idhini wakurugenzi hao wakuu kubainisha malipo ya Wakurugenzi Wakuu wasiokuwa Watendaji.

**Kama shughuli maalum ya kuzingatia na, ikipatikana kufaa, kupitisha maamuzi yafuatayo:**

**5. Kama uamuzi wa kawaida:**

**KWAMBA** wakurugenzi wakuu wafuatao ambao wametimu umri wa miaka 70 kuendelea kuhudumu kama wakurugenzi wakuu wa Kampuni:

- a) "Kwamba Dkt Wilfred Kiboro, akiwa mkurugenzi anayestaafu kulingana na Kifungu cha 101 cha Muafaka wa Maelewano ya Kampuni na ambaye amezidi umri wa miaka 70, bila kuzingatia suala hilo, atachaguliwa kama mkurugenzi mkuu wa Kampuni hii kwa kipindi cha mwaka mmoja."
- b) "Kwamba Prof Lee Huebner, mkurugenzi mkuu anayestaafu kulingana na Kifungu cha 101 cha Muafaka wa Maelewano ya Kampuni na ambaye amezidi umri wa miaka 70, bila kuzingatia suala hilo achaguliwe tena kama mkurugenzi mkuu wa Kampuni hii kwa kipindi cha mwaka mmoja."
- c) "Kwamba Bw Anwar Poonawala, mkurugenzi mkuu anayestaafu kulingana na Kifungu cha 101 cha Muafaka wa Maelewano ya Kampuni na ambaye amezidi umri wa miaka 70, bila kuzingatia suala hilo, achaguliwe tena kama mkurugenzi mkuu wa Kampuni hii kwa kipindi cha mwaka mmoja"
- d) "Kwamba Bw Francis O. Okello, mkurugenzi mkuu anayestaafu kulingana na Kifungu cha 101 cha Muafaka wa Maelewano ya Kampuni na ambaye amezidi umri wa miaka 70, bila kuzingatia suala hilo, achaguliwe tena kama mkurugenzi mkuu wa Kampuni hii kwa kipindi cha mwaka mmoja"

**6. Kama uamuzi maalum:**

"**KWAMBA** kifungu kipya kitakachotajwa kama Kifungu cha 13A kimechopekwa mara moja katika Muafaka wa Maelewano ya Kampuni kufuatia Kifungu cha sasa cha 13 jinsi ifuatavyo: 13A. Kampuni hii inaweza kununua hisa zake yenyewe kulingana na Sehemu ya XVI ya Sheria ya Kampuni ya 2015."

**7. Kama uamuzi maalum:**

"**KWAMBA** kifungu kipya kitakachoitwa Kifungu cha 68A kimechopekwa mara moja katika Muafaka wa Maelewano wa Kampuni kufuatia Kifungu cha sasa cha 68 jinsi ifuatavyo:

- a) kuitisha mkutano wa wenyehisa, wote kufanyika kwa njia mawasiliano ya kielektroniki; au
- b) kutoa fursa ya mwenyehisa mmoja au zaidi, au wawakilishi wa wenyehisa kushirika kwa njia ya kielektroniki katika mkutano mzima au nusu yake, mkutano ambao unaendeshwa kwa njia ya ana kwa ana, almradi mawasiliano hayo ya kielektroniki kwa kawaida yanawawezesha watu wote wanaoshiriki katika mkutano huo kuwasiliana kwa wakati mmoja na wenzao bila kuhusisha mtu wa kati, na kushiriki kwa ufaafu wa kuridhisha katika mkutano huo.

68A(ii) Iwapo ushiriki wa wenyehisa katika mkutano ni wa njia ya mawasiliano ya kielektroniki, jinsi ilivyotarajiwa katika katika Kifungu cha 68A(i)

- a) ilani kuhusu mkutano huo sharti iwafahamishe wenyehisa kuhusu uwepo wa fomu za ushiriki, na kutoa maelezo yoyote yanayohitajika ili kuwawezesha wenyehisa au wawakilishi wao kupata mbinu au njia za mawasiliano ya kielektroniki; na
- b) ufikiaji wa mbinu au njia ya mawasiliano ya kielektroniki ni kwa gharama ya mwenyehisa au mwakilishi wake, isipokuwa katika hali ambapo Kampuni inaamua vinginevyo.

**8. Kama uamuzi maalum:**

"**KWAMBA**, kulingana na Sehemu ya 458 ya Sheria ya Kampuni, 2015, Kampuni hii inatakiwa na inaidhinisha kufanya ununuzi wa hisa wa hisa za kawaida zilizolipiwa na kutolewa za KES 2.50 kwa kila moja kwenye soko la hisa za Kampuni ("**Hisa za Kawaida**") kulingana na **ununuzi-wa-ulichouza** kwa Hisa za Kawaida kwa mujibu wa masharti na sheria zilizoorodheshwa katika Ilani kwa wenyehisa wa Kampuni hii iliyotolewa Jumatatu tarehe 31 Mei 2021 (ununuzi-wa-ulichouza") na ambayo ilani hiyo ilitolewa kwa wenyehisa kwa pamoja na ilani ya mkutano mkuu wa mwaka (na pia inapatikana katika tovuti ya Kampuni), almradi:

- (a) idadi ya juu zaidi ya Hisa za Kawaida zinazoweza kununuliwa kulingana na masharti ya uamuzi huu ni 20, 739,652 ya Hisa za Kawaida.;
- (b) bei ya juu zaidi inayoweza kutolewa kwa Hisa yoyote ya Kawaida itakuwa KES 25.00 jinsi ilivyopendekezwa ba Bodi;
- (c) bei ya chini zaidi inayoweza kulipwa kwa Hisa yoyote ya Kawaida itakuwa KES2.50 ikiwa ndiyo thamani iliyotajwa ya hisa; na
- (d) agizo hili litakoma kutumika mwishoni mwa miezi 18 kuanzia tarehe ya mkutano mkuu wa mwaka wa Kampuni utakaofanyika Ijumaa, tarehe 25 Juni 2021, isipokuwa awali ikiwa imebadilishwa, kufutiliwa mbali au kupangwa upya kulingana na kanuni za Sheria ya Kampuni ya 2015."

**9. Kama uamuzi maalum:**

"**KWAMBA**, kulingana na sehemu ya 329 ya Sheria ya Kampuni ya 2015 wakurugenzu wakuu wa Kampuni hii waidhinishwe kijumla na bila masharti kuzigawa upya Hisa hizo za Kawaida jinsi zilivyonunuliwa na Kampuni hii kulingana na Ununuzi-wa-Ulichouza mradi tu kwamba agizo hili lita, isipokuwa likifanywa upya, litabadilishwa au kufutiliwa mbali na Kampuni, kupitwa na wakati kabla ya miaka mitano kuanzia tarehe ya maamuzi haya."

**10.** Shughuli nyingine yoyote ambayo imetajwa kwenye Ilani halisi iliyotolewa.

**Kwa Amri ya Bodi**

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni

**31 Mei 2021**

**FAHAMU:**

1. Kulingana na kanuni za sehemu ya 3 ya Sheria ya Kampuni ya 2015 kama ilivyorekebishwa kupitia kwa Sheria ya Sheria za Biashara (Zilizorekebishwa) (Namba 2), 2021, Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) wa Hamsini na Nane wa shirika la Nation Media Group PLC ("Kampuni") utafanyika kwa njia ya kielektroniki Ijumaa tarehe 25 Juni 25 2021 saa tisa mchana.

2. Wenyehisa ambao wangependa kushiriki katika mkutano huo wanafaa wajisajili kwa AGM kwa kubofya nambari ***483*822#** kupitia kwa laini yoyote ya simu na kufuata maelekezo mbalimbali kuhusiana na harakati hiyo ya usajili. Ili kukamilisha harakati ya usajili, wenyehisa watahitajika wawe na Nambari zao za Vitambulisho vya Kitaifa/Paspoti na/au Nambari zao za Akaunti za CDSC zilizotumika wakati wa ununuzi wa hisa zao. Kwa usaidizi wenyehisa (wawe Wakenya au wageni) wapige simu kwa kubofya nambari zifuatazo za usaidizi: (+254) 709170 000 kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni, Jumatatu hadi Ijumaa. Mwenyehisa aliye nje ya Kenya anaweza kutuma baruapepe yake kwa Image Registrars kupitia kwa **NMGAGM@image.co.ke.**

3. Kujisajili kwa ajili ya ATM kunafunguliwa tarehe 31 Mei 2021 saa tatu asubuhi na kutafungwa Jumanne tarehe 22 Juni, 2021 saa kumi na moja jioni.

4. Kulingana na Sehemu ya 283 (2) (c) ya Sheria ya Kampuni, nakala zifuatazo zinaweza kutazamwa/kupatikana kwenye tovuti ya Kampuni **https://www.nationmedia.com** (i) nakala ya Ilani hii na fomu ya uwakilishi; (ii) taarifa za kifedha za kampuni zilizkaguliwa za mwaka wa 2020; (iii) Nakala ya Muafaka wa Maelewano Uliorekebishwa.

5. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali au kupata ufanunuzi kuhusiana na Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) wanaweza kufanya hivyo kwa:
   - a) Kutuma maswali yao kwa njia ya maandishi kwa **NMGAGM@image.co.ke**
   - b) wenyehisa watakaokuwa wamesajiliwa kushiriki katika mkutano huo wataweza kuuliza maswali kwa njia ya ujumbe mfupi/arafa (sms) kwa kubofya nambari msimbo USSD iliyotajwa hapo juu na kuchagua (Ask Question) kwenye kiulizo
   - c) ikiwezekana, kuwasilisha maswali yaliyoandikwa kwa njia ya mkono yakiwa na anwani ya mahali aliko muulizaji au anwani ya baruapepe kwa Image Registrars Limited, orofa ya 5 jumba la Absa Towers (awali likiitwa Barclays Plaza), barabara ya Loita Street, Nairobi, au
   - d) Nairobi kutuma maswali yao yaliyoandikwa yakiwa na anwani ya mahali aliko muulizaji au baruapepe yake kwa njia ya posta kwa anwani ya Kampuni S.L.P 58485-00200, Nairobi.

   Sharti wenyehisa watoe maelezo yao kwa ukamilifu (majina kamili, Nambari za Kitambulisho/Paspoti/Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapowasilisha maswali yao au maombi ya ufafanuzi.

   Maswali yote na maombi ya ufafanuzi sharti yafikie Kampuni siku ya au kabla ya Jumatano tarehe 23 Juni, 2021 saa tano adhuhuri.

   Baada ya kupokea maswali na maombi ya ufafanuzi, wakurugenzi wakuu wa Kampuni hii watatoa majibu kwa njia ya maandishi kupitia kwa anwani au baruapepe zilizotolewa na Wenyehisa katika muda usiozidi saa 12 kabla ya kuanza kwa mkutano mkuu. Orodha kamili ya maswali yote yaliyopokelwa na majibu yake itachapishwa kwenye tovuti ya Kampuni katika muda usiozidi saa 12 kabla ya kuanza kwa mkutano mkuu.

   Kulingana na Sehemu ya 298(1) ya Sheria ya Kampuni, wenyehisa wanaofuzu kushiriki na kupiga kura katika AGM hiyo wanaruhusiwa kuteua wawakilishi wao ili wapige kura kwa niaba yao. Si lazima mwakilishi kama huyo awe mwanachama wa kampuni. Fomu ya uwakilishi imeambatishwa kwenye Ilani hii na inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni hii kupitia linki: **https://www.nationmedia.com.** Nakala za karatasi za fomu ya uwakilishi pia zinapatikana kupitia kwa anwani: Image Registrars Limited offices, Orofa ya 5 jumla la Absa Towers (awali likiitwa Barclays Plaza), barabara ya Loita Street. Sharti fomu ya hiyo ya uwakilishi itiwe saini na mteuzi au wakili wake aliyeidhinishwa kwa njia ya maandishi. Iwapo mteuzi ni shirika, shirika hilo linalomteua mwakilishi huyo litahitajika kuweka saini ya afisa au wakili aliyeidhinishwa na shirika hilo. Fomu iliyojazwa ya uwakilishi itumwe kwa **NMGPAGM@image.co.ke.** Au iwasilishwe kwa Image Registrars Limited offices, Orofa ya 5 jumla la Absa Towers (awali likiitwa Barclays Plaza), barabara ya Loita Street, S.L.P 9287-00100 GPO, Nairobi ili ipokelewe kabla ya Jumatano tarehe 23 Juni 2021 saa tisa mchana. Mtu yeyote aliyeteuliwa kama mwakilishi anafaa awasilishe nambari yake ya simu kwa Kampuni hii kabla ya Alhamisi tarehe 24 Juni 2021 saa nne asubuhi. Usajili wowote wa mwakilishi utakaokataliwa utaarifiwa kwa mwenyehisa anayehusika kabla ya tarehe 24 Juni 2021 ili kuruhusu muda wa kusuluhisha masuala ibuka.

6. Mkutano Mkuu utapeperushwa kielektorniki moja kwa moja kupitia linki ambayo itatolewa kwa wenyehisa watakaokuwa wamejisajili kushiriki katika mkutano huo mkuu. Wenyehisa waliosajiliwa pamoja na wawakilishi wao watapokea ujumbe mfupi (sms/USSD) kwenye nambari yao ya simu iliyosajiliwa, saa 24 kabla ya Mkutano huo Mkuu, ujumbe utakaotumika kama ukumbusho kuhusu AGM. Ujumbe mfupi wa pili (SMS/USSD) utatumwa saa moja kabla ya AGM, ukiwakumbusha wenyehisa waliojisajili na wawakilishi wao kuwa AGM itaanza katika muda was aa moja na kutoa linki ya mawasiliano ya mkutano ya moja kwa moja.

7. Wenyehisa waliosajiliwa na wawakilishi wao watafuatilia mkutano huo wa AGM kwa kutumia jukwaa la kielektroniki la moja kwa moja na wanaweza kupata ajenda zake pia. Wenyehisa hao waliosajiliwa pamoja na wawakilishi wanaweza kupiga kura (watakapoitishwa kufanya hivyo na mwenyekiti) kupitia USSD.

8. Kura ya maoni itafanywa kuhusu kila mojawapo ya maamuzi yatakayotolewa katika ilani.

9. Matokeo ya AGM yatachapishwa kwenye tovuti ya Kampuni katika muda usiozidi masaa 24 baada ya kukamilika kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

OUR BRANDS
DAILY NATION | DAILY MONITOR | RWANDA TODAY | Mwana Spoti | NTV | dembe fm | Nation Sema | Pishi | Lit 360 | TAG brand studio | KUSI IDEAS FESTIVAL
BUSINESS DAILY | MWANANCHI | THE CITIZEN | ntv | Spark TV | NATIONFM | KFM | NAIROBI NEWS | KENYA BUZZ | Nation ePaper | NATION Empower Africa
The EastAfrican | TAIFA LEO | ENNYANDA